Mambo 10 unayopaswa kujua kuhusu COVID-19 na Watu wenye Ulemavu

Kikundi cha Wafanyakazi wa Kiufundi cha Save the Children Inayojumuisha Watoto wenye Ulemavu, Tarehe 18, Machi

Katika nchi kadhaa na kwa kiwango cha ulimwengu, watu wenye ulemavu wamesema kwamba taarifa za serikali hazisambazwi kwa njia zinazopatikana au hatua hazichukuliwi ili kufidia upunguzwaji wa huduma za msaada ambazo watu wenye ulemavu hutegemea. Mwandishi Umoja wa Mataifa wa haki za watu wenye ulemavu ametoa taarifa ambayo inaweza kusomwa hapa.

1. **Jitihada zote za kukabiliana na utayari wa dharura zinahitaji kuwa jumuishi**
   Ni muhimu kuhakikisha kuwa juhudi zote za kuzuia kuenea kwa virusi na za kudhibiti waliougua ni jumuishi. Programu jumuishi ni pamoja na **uhamasishaji wa ufahamu** kwa hali ya watu na watoto walemavu na homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19). Pia inajumuisha **kufanya taarifa zote na shughuli kupatikana** ili kuwafaidi kwa usawa watu wazima na watoto wenye ulemavu kama inavyowafaidi watu wengine. **Baadhi ya hatua zinahitaji kulenga watu wenye ulemavu**, kama vile hatua ya ulinzi wa kijamii ili kudumisha mwendelezo katika miundo ya msaada. Unaweza kupata miongozo ya IASC juu ya kujumuisha watu wenye ulemavu katika hatua za kuzingatia ubinadamuhapa. Mengi yanatumika katika mipangilio yote.

2. **Watu wenye ulemavu na mashirika yao wakilishi lazima washirikishwe katika hatua zote za majibu**
   Watu wenye ulemavu ndio wataalamu wa kweli katika jinsi ya kujumuisha vikundi vilivyo na changamoto tofauti katika juhudi zote za majibu, utayari, taarifa na utoaji wa huduma. Harakati ya wenye uluemavu ina kauli mbiu ya 'Hakuna cha Kutuhusu Sisi Bila Sisi' ili kuimarisha ujumbe kwamba mambo yote yanayofanywa kukuza haki za watu wenye ulemavu yanahitaji kujumuisha watu wenye ulemavu. Hii ni kweli haswa nyakati za hatari ambapo hatua za kulinda vikundi vilivyotengwa na vinavyokumbana na unyanyapaa mara nyingi huachwa nyuma. Unaweza kupata orodha ya mashirika wakilishi katika mataifa mengi tunayoyafanyia kazihapa.

3. **Watu wenye ulemavu ni mojawapo ya kundi lililo katika hatari kubwa**
   Ingawa ulemavu wenyewe haumuweki mtu katika kundi lenye hatari kubwa, watu wenye ulemavu wana uwezekano wa kuwa na hali mbaya za kiafya ambazo zinaweza kuzidisha athari za virusi. Taarifa kuhusu virusi vya corona zipo kila mahali lakini bado ni kidogo kuhusu kile cha kufanya ikiwa uko katika kundi lililo katika hatari kubwa, hivyo kupelekea idadi kubwa ya simu kutoka kwa watu wenye ulemavu wakiwa na wasiwasi mwingi.

4. **Kusema "Usiwe na wasiwasi, ni hatari kwa wazee na wagonjwa au wale walio na hali mbaya ya kiafya " hakufai**
   Aina hii ya kujieleza haiambatani na mtazamo wa haki za kibinadamu. Save the Children, kama shirika, linaunga mkono, sio tu Mkataba wa Haki za Watoto, lakini pia, haki za watu wote ulimwenguni, na Mkataba wa watu wenye ulemavu. Maelezo hayo pia yanashusha umuhimu wa uangalifu wa kuzuia kuenea kwa virusi. Ni muhimu kuwalinda watoto wenye ulemavu zaidi na wa hali ya juu kutokana na ujumbe kama huu ambapo wanarejelewa kama sehemu ya jamii iliyo 'ugua' au 'dhaifu' kwani hii inaathiri vibaya hali yao ya kujiamini.

5. **Jumbe za afya ya umma ni LAZIMA utolewe kwa njia tofauti na zinazofikiwa**
   Kwa sababu watu wanawasilisha na kuelewa maelezo kwa njia tofauti, ni muhimu kutoa maelezo kupitia njia kadhaa za mawasiliano. La sivyo, mambo yanaweza kuharibika. Taarifa zinatakiwa pia kuwa katika mfumo wa watoto kuelewa , maelezo yanapaswa kujumuisha sauti, chapisho kubwa, linalosomeka kwa urahisi, picha na lugha ya ishara. Nambari za kupata maelezo zinapaswa kuwa katika njia ya maandishi na barua pepe kwa wale walio na matatizo wa kusikia. Tazama mifano katika kila kiungo.

6. **Ratiba zilizovurugika zinaweza kuwa ngumu kwa watoto wanaougua ugonjwa wa usonji , au wengine ambao wanahitaji ratiba zinazoaminika.**

Ratiba ya kila siku inapovurugika, kama vile kutoenda shuleni, kutoenda kwenye matembezi ya kila siku au kuweza kupata chakula cha kawaida, familia zilizo na watoto wenye ulemavu zinaweza kupata shida kubwa na mara nyingi zinaweza kuhitaji msaada wa ziada. Watoto au wazazi wengi wamezoea mipangilio fulani ambayo, inapovurugika, inaweza kusababisha changamoto nyumbani na zaidi kuwaweka watoto wenye ulemavu na ndugu zao katika hatari kubwa ya kubughudhiwa au unyanyasaji.

7. Kupata dawa ya kawaida inaweza kuwa ngumu zaidi

Watoto wengi wenye ulemavu wanahitaji dawa za mara kwa mara ili kubaki wenye afya na wachangamfu. Mifumo ya afya inapovurugika na kliniki za afya kupungukiwa na uwezo wa kutoa huduma bora, watoto wenye ulemavu wanaweza kukosa dawa muhimu yenye kuwafanyawenye afya. Hii ni kweli haswa ikiwa huduma za afya tayari zinabagua watu wenye ulemavu kwa sababu ya unyanyapaa unaotokana na dhana potofu, au ukosefu wa ufahamu.

8. Watu wenye ulemavu wanaweza kushindwa kufuata tahadhari zilizopendekezwa za jinsi ya kujikinga

Watu wengi wenye ulemavu hutegemea msaada kutoka kwa wengine ili kufanya vitu wakati wa mchana. Hii ni pamoja na kunawa mikono, kula, kuvaa, kushikilia kitu ili kufunika mdomo wanapopiga chafya, kutupa tishu, kufua nguo n.k. Unapohitaji mtu kukusaidia katika ratiba yako ya kila siku, inaweza kuwa haiwezekani kujitenga katika shughuli za mchana kutwa, au hata kwa kufanya maandalizi ya kutokaribiana na wengine. Kununua na kuhifadhi mboga, au kufikisha mboga nyumbani wakati pia unahitaji msaada unakuwa changamoto nyingine. Watoto haswa wako hatarini, lakini pia watoto wadogo wa wazazi wenye ulemavu wanaweza kuathiriwa.

9. Mlipuko wa Virusi vya Korona unaweza kupunguza hali ya kujitegemea na kuongeza mazingira hatarishi.

Msaada wa kibinafsi ni muhimu kwa watu wengi wenye ulemavu ili kuwawezesha kuishi kwa kujitegemea. Karantini na hali ya kukaa mbali na wengine zinaweza kudhoofisha mfumo wa msaada unaolenga kusaidia watu wenye ulemavu kuishi kwa kujitegemea nyumbani. Maisha ya kila siku yanaweza kuathiriwa zaidi ikiwa wafanyakazi muhimu au wanafamilia wameambukizwa na kwa hivyo kushindwa kufanya kazi zao za msaada kama kawaida. Sote tumesikia kuhusu mvulana mwenye umri wa miaka 16 nchini China, ambaye alikuwa akiishi na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo na akafa kutokana na kupuuzwa, wakati baba yake aliwekwa kwenye karantini bila kutarajia, na bila kupangia maslahi ya mtoto wake. Uamuzi wa kujiweka mwenyewe, pamoja na msaidizi katika hatari unazidisha ugumu wa hali hiyo. Hii ni kweli hasa katika sehemu za makazi. Kukata mawasiliano na wapendwa pamoja na miundo ya msaada inaweza kuwaacha watu wenye ulemavu, haswa watoto, katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa aina yoyote.

10. Kufungwa kwa shule za mabweni na vituo vya siku kunaweza kuwaweka watu wenye ulemavu kwenye hatari ya kudhulumiwa

Iwapo shule za makazi na vituo vya mchana zitafungwa au huduma kughairiwa, mipango inapaswa kuwekwa ili kuimarisha utunzaji wa nyumbani na katika shughuli. Kwa kuwa watoto wenye ulemavu wanaweza kuhitaji utunzaji wa ziada ukilinganisha na watoto wengine, familia ambazo hazijazoea kukaa na mtoto nyumbani wakati wote zinaweza kuhangaika , na kupelekea mtoto kuwa katika hatari ya kunyanyaswa, kupuuzwa na dhuluma. Mabadiliko ya ghafla na yasiyotarajiwa kutoka kwa watoa huda wa msingi, na mifumo ya usalama, yanaweza kusababisha madhara ya kisaikolojia kwa mtoto.